

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

29 OKTOBA, 2021

TAARIFA KWA UMMA

MANISPAA YA KINONDONI YA IMEIDHINISHA MIKOPO YA WANAWAKE VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU ROBO YA NNE YA MWAKA 2020/2021

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kuitia Kamati yake ya Fedha na Uongozi imeidhinisha kiasi cha Tshs. **266,875,000/=** fedha za mfuko wa wanawake, vijana na Watu wenyе Ulemavu kwa vikundi **57** vyenye sifa baada ya kukidhi vigezo vyote vinavyotakiwa na kanuni mpya ya mwaka **2021** inayotumika katika utoaji wa mikopo hiyo.

Taarifa iliyotolewa na kamati ya mikopo katika kikao cha Kamati ya Fedha na Uongozi inaonesha kuwa Tshs. **142,900,000/=** zimetolewa kwa vikundi **32** vya wanawake, Tshs. **64,200,000/=** zimetolewa kwa vikundi **19** vya vijana na Tshs. **59,775,000/=** zimetolewa kwa vikundi **6** vya watu wenyе ulemavu.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Mh. Songoro Mnyonge ametoa rai kwa wananchi wa Kinondoni, hususani Wanawake, Vijana na Watu wenyе ulemavu kuitumia fursa hii iliyotolewa na Serikali kuinua kipato chao. Pia ameitaka Menejimenti ya Manispaa na Idara husika kuongeza kasi na umakini katika uhakiki wa Vikundi vya waombaji ili fedha inayotokana na **10%** ya Mapato ya ndani zinazotengwa kila mwezi ziweze kutolewa zote na kuwafikia waombaji wote kwa wakati katika kila robo ya mwaka.

Akizungumzia tatizo la marejesho ya Mikopo inayotolewa kwa vikundi hivyo, Mstahiki Meya amewataka Waheshimwa Madiwani wote na wataalam kuangalia namna nzuri ya kubuni miradi kwani ni vema kuwa na vikundi vichache vyenye mkopo wenyе tija ili ili miradi inayoanzishwa na Vikundi iwe na faida kwa wananchi na itakayowezesha kurejeshwa kwa Mkopo uliotolewa kwa wakati bila vikwazo.

Jumla ya vikundi **72** vyenye thamani ya Tshs. **618,252,330/=** viliomba mikopo hiyo katika robo ya nne **2020/2021**, wanawake vikundi **39** vyenye thamani ya Tshs. **265,300,000/=**, Vijana vikundi **27** vyenye thamni ya Tshs. **293,177,333/=** na watu wenyе ulemavu vikundi **6** vyenye thamani ya Tshs. **59,777,000/=**.

Imetelewa na:

Sebastian M. Mhowera
AFISA UHUSIANO
MANISPAA YA KINONDONI